



## مجلة جامعة السميٲ

مجلة محكمة نصف سنوية يصدرها مركز البحوث والدراسات العليا

## SUMAIT University Journal (SUJ)

A peer-reviewed biannual journal published by the Center of  
Research and Postgraduate Studies (CRPS)

---

ISSN: 2507-7864

السنة الرابعة، العدد التاسع، ديسمبر 2021  
Fourth Year, Issue No. 9, December, 2021

# Taswira ya Misri Katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili

Wael Nabil Ibrahim Othman

Profesa Mshiriki wa Fasihi ya Kiswahili, Idara ya Lugha za Kiafrika

Kitivo cha Lugha na Ufasiri, Chuo Kikuu cha Al Azhar, Misri.

Dr.Wael\_Nabil@Azhar.edu.eg

*Received: 22 Jun 20221, Accepted: 30 September 2021, Published December 2021*

© SUMAIT University Journal 2021

---

## Abstract:

The relationship between Egypt and East Africa dates to the fifteenth century B.C., during the reign of Queen Hatshepsut, when she sent a commercial ship to Punt, bringing incense and ivory. East Africa was part of Punt, and archeology supported this view, although some scholars have argued that Punt countries are located in the North East region of Africa, namely, Somalia and Ethiopia. Thus, this historical connection had a profound effect on the hearts of Kiswahili writers, as they described many things about life and general conditions in Egypt through their Novels. This paper studied and analyzed these Novels in depth.

**Keywords:** Literature, Travel, Imagery, Egypt, Novel, Swahili.

**Ikisiri:** Uhusiano kati ya Misri na Afrika Mashariki umeanza mnamo karne ya kumi na tano K.K. takriban, wakati wa enzi za Malkia Hatshepsut, ambaye alipeleka meli ya kibiashara kwenda Punt, ikileta uvumba na meno ya Tembo. Afrika Mashariki ilikuwa sehemu ya Punt, na akiolojia iliunga mkono maoni haya, ingawa baadhi ya wasomi walikuwa wakieleza kwamba nchi za Punt ziko kwenye eneo la Kaskazini Mashariki mwa Afrika, ambaloni, Somalia na Ethiopia. Kwa hivyo, uhusiano huu wa kihistoria ulikuwa na athari kubwa katika mioyo ya waandishi wa Kiswahili, kwani walielezea mambo kadhaa kuhusu maisha na hali ya jumla huko Misri kupitia riwaya zao. Makala haya yana kusudio la kuchambua riwaya hizi kwa undani.

**Maneno Makuu:** Fasihi, Safari, Taswira, Misri, Riwaya, Kiswahili.

## 1.0 Utangulizi

Mbatia (2001: 18) aliifafanua istilahi ya “Fasihi ya Usafiri,” katika kamusi yake ya fasihi akieleza kuwa ni:

“Masimulizi ambayo aghalabu hutolewa na mtunzi mwenyewe juu ya tajiriba zake akiwa safarini. Mara nyingi, masimulizi kama hayo yanahusu mambo yaliyomshangaza, kumtumbuiza au kumwelimisha msimulizi.”

Mbatia alitaja mifano miwili ya Fasihi ya Usafiri katika Kiswahili: Riwaya ya *Tulichokiona na Tulichokifanya Ingereza* iliyoandikwa na H.M.T. Kayamba, na *Safari yangu ya Urusi na Siberia*,

iliyoandikwa na Salim Bin Abakari, akionesha kuwa riwaya hizi mbili zimesheheni maelezo kuhusu mambo ya kustaajibisha ambayo wasimulizi waliyaona katika nchi hizi za kigeni walizozitembelea (Mbatia 2001: 18).

Ikumbukwe pia kwamba Madumulla (2009: 42) alipogusia suala la historia ya riwaya ya Kiswahili Tanzania na mikondo yake, ameeleza kuwa riwaya ya Kiswahili ina mikondo kadhaa, miongoni mwa mikondo hii ni Mikondo ya kisafari na kimaadili. Katika maelezo yake alitaja mfano wa kitabu cha Tipp Tip: *Maisha ya Hamed Bin Mohammed El Murjebi au Tipp Tip, Kwa Maneno Yake Mwenyewe*.

Wakati Wamitila (2008: 115) alipotaja Riwaya ya Safari, alisema:

“Katika riwaya ya aina hii, motifu ya safari au kusafiri kutoka sehemu A hadi D (kupitia B na C) huchukua nafasi kubwa sana.”

Kwa hivyo, ni wazi kuwa Fasihi ya Usafiri iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili ni hadithi zilizosimuliwa na mwandishi, akiandika ndani yake kila kitu alichooona na kujifunza wakati wa kusafiri. Waswahili wengi wameandika kutoka nyakati za zamani kile walichokiona katika safari zao, kwa mfano:

- Sleman bin Mwinyi Tshande bin Mwenyi Hamisi esh Shirazi, aliyeandika *Safari Yangu ya Bara Afrika* katika karne ya kumi na tisa (Velten, 1901:281).
- Selim bin Abakari, aliyeandika *Safari Yangu ya Nyassa, Safari Yangu ya Ulaya Toka Daressalama Hata Berlin*, na *Safari Yangu ya Russia* katika karne ya kumi na tisa (Velten, 1901:281).
- Mtoro bin Mwinyi Bakari, aliyeandika *Safari Yangu Udoe hata Uzigua*, na *Khabari ya Nchi za Wazaramu na Desturi za Wazaramu*, katika karne ya kumi na tisa (Velten, 1901:281).
- Abdallah bin Rashid aliyeandika *Safari Yangu ya Afrika*, katika karne ya kumi na tisa (Velten, 1901:281).
- Tipp Tip aliyeandika kitabu chake *Maisha ya Hamed Bin Mohammed El Murjebi au Tipp Tip, Kwa Maneno Yake Mwenyewe*. Kilichoandikwa kwa namna ya kinudhumu na kinathari kuhusu safari zake za Tanganyika na Congo mwishoni mwa karne ya 19 (Madumulla, 2009: 42).
- Kayamba aliyeandika kitabu chake *Tulivyoona na Tulivyofanya Ingereza*, kilichochapishwa Uingereza mwaka wa 1932. (Kayamba, 1932)

Hivi karibuni, kuna waandishi wengi wa fasihi ya Kiswahili ambao wameandika katika aina hii ya fasihi, miongoni mwao ni:

- John Habwe aliyeandika riwaya ya *Safari ya Lamu*, iliyochapishwa Nairobi, 2011. (Habwe, 2011)
- Shafi Adam Shafi aliyeandika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, iliyochapishwa Nairobi mwaka wa 2013. (Shafi, 2013)

- Rocha Chimera aliyeandika riwaya ya *Siri Sirini*, iliyochapishwa Nairobi mwaka wa 2013. (Chimera, 2013)

## 2.0 Data za Makala

Data za makala haya zimekusanywa kutoka katika riwaya mbili; *Mbali na Nyumbani* na *Siri Sirini* zilizotajwa hapo juu, ambapo kila mwandishi wa riwaya hizi amechora picha ya Misri katika riwaya yake kwa kadri alivyoiona kwa mtindo wa kifasihi.

### 2.1 *Mbali na Nyumbani* na Mwandishi wake

Riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ina kurasa 482. Riwaya hii ina Sura 44. Kila Sura ina kichwa kinachoelezea yaliyomo ndani yake. Kwa hivyo, kila Sura inawakilisha hatua muhimu katika safari ya mwandishi. Inabainika kuwa idadi ya kurasa sio sawa katika kila Sura, hii imetokana na kutokulingana kwa idadi na mfululizo wa matukio katika Sura hizo, kwa hivyo matukio zaidi na zaidi katika kila Sura husababisha kuongezeka kwa idadi ya kurasa zake, na kinyume chake.

Inaeleweka kutokana na Jina la Riwaya hii kwamba inazungumzia motifu ya kusafiri nje ya nchi. Mwandishi alianza kukusanya kumbukumbu zake za kusafiri, kwa kuziandika mnamo mwaka wa 2001 BK. Wakati huo alipomuahidi binti yake kuwa atatumia muda wake kwa kuandika maelezo ya safari yake kutoka nchini mwake kwenda Uingereza kumaliza masomo yake huko. Hayo yalitokea mnamo Mwezi wa Aprili 1960 BK, ambapo ukoloni wa Uingereza bado ulikuwa ukitawala Zanzibar.

Wakati huo Shafi alikuwa bado ni mwanafunzi katika Chuo cha Ualimu Zanzibar katika eneo la Beit-el-Ras, pembezoni mwa Bahari ya Hindi, ambapo alikuwa mara kwa mara akiangalia meli zinazopita, huku alitamani kusafiri, mwishowe aliamua kusafiri kwenda Aden na kutoka huko hadi Mombasa nchini Kenya.

Baada ya kukaa Mombasa na Nairobi kwa siku kadhaa, aliendelea na safari yake, akipita Uganda kisha akafika mji mkuu wa Sudan, Khartoum, hadi Kairo ambako alijiunga na Kambi ya Jeshi la Misri na kupata mafunzo ya kijeshi. Shafi alirudi Zanzibar siku ya Juni mosi 1961. Safari hii ilichukua mwaka mzima. Mnamo mwezi wa Agosti mwaka huo huo alisafiri tena kwenda Nairobi na kutoka huko alikwenda mji mkuu wa Ujerumani Berlin. Huko pia alipata mafunzo ya kijeshi na alijifunza lugha ya Kijerumani kisha akarudi Zanzibar. Baada ya miaka arobaini na nne, na hasa mnamo Mwezi wa Oktoba 2005, Shafi alikwenda katika mji mkuu wa Uganda Kampala, ambako alihudhuria Tamasha la kuwaenzi waandishi wa Kiafrika lililoandaliwa na Kituo cha Uingereza. Mnamo 2009, alimaliza kuandika riwaya yake hii ya kitawasifu.

Shafi ni mwandishi maarufu sana wa riwaya nchini Tanzania. Alizaliwa mjini Zanzibar mwaka 1940. Baada ya kupata elimu yake ya shule ya msingi alijiunga na Chuo cha Ualimu cha Seyyid Khalifa (Baadae Chuo cha Ualimu cha Nkurumah na sasa ni Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)) mwaka 1957 hadi mwaka 1960. Alipata Diploma ya juu katika fani ya Siasa ya Uchumi katika Chuo cha Fritz Heckert katika iliyokuwa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Ujerumani mwaka 1963. Alipata mafunzo ya uandishi wa habari mjini Prague, nchini Czechoslovakia (sasa Jamhuri ya Czech) mwaka 1964 hadi mwaka 1965, nchini Sweden

mwaka 1982 na nchini Marekani mwaka 1983. Adam Shafi alikuwa Mwenyekiti wa Umoja wa waandishi wa vitabu Tanzania (UWAVITA) kuanzia 1998 hadi 2002. Alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Maendeleo ya Vitabu Tanzania, (BAMVITA) mwaka 2002.

Shafi ameandika riwaya nyingi zikiwemo: *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978), *Kuli* (1979), *Vuta n'kuvute* (1999), *Haini* (2003), *Mbali na Nyumbani* (2013), na *Mtoto wa Mama* (2018)."

## 2.2 Siri Sirini na Mwandishi wake

Riwaya ya *Siri Sirini* ina juzuu tatu: Juzuu ya kwanza ambayo makala haya yameitegemea, anwani yake ni *Mshairi na Mfungwa*, ina kurasa 403. Juzuu hii ina sura ishirini, kila sura ikiwa na nambari na isiyo na kichwa, na kurasa 54 zilizoambatanishwa nayo kuelezea maneno Magumu. Hata hivyo, msomaji wa riwaya hii, hugundua kuwa sura zake zinaendelea, zinaibuka kwa matukio, zinategemeana, na zina uhusiano wa kawaida. Kwa hivyo haiwezekani kutenganishwa sura moja na nyingine, na inaonekana kuwa mwandishi alijumuisha ndani yake maono yake ya kibinafsi na uzoefu wake wa kibinadamu, na kwa hivyo, ni kazi ya fasihi kamili.

Sehemu ya kwanza ya Riwaya hii inahusu kuwekwa kizuizini kwa Fumo Liyongo ambaye ni mshairi mashuhuri wa Waswahili. Kufungwa kwake katika mji wa Shanga, kisha kutoroka kwake kwenda mji jirani wa Ozi. Inazungumzia pia safari ya ujumbe wa serikali ya Shanga kwenda Misri, na kila pahala ambapo wajumbe hawa walipoona kuanzia kufikia kwao Misri hadi kurudi kwao mji wa Shanga, na hiyo ndiyo maudhui kuu ya makala haya.

Chimera ni mwandishi wa Kenya. Alipokea Tuzo la Noma mnamo mwaka 2000 kwa Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu (1999) alichokitunga pamoja na Kimani Njogu. Chimera amepata Shahada yake ya Elimu (B.ED.) na ya Uzamili (M.A.) kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta, na amepata shahada yake ya Uzamivu (Ph.D.) kutoka Chuo Kikuu cha Ohio. Yeye ni Profesa wa Kiswahili na mwenyekiti wa zamani wa Idara ya Lugha na Isimu katika Chuo Kikuu cha Egerton. Hivi sasa, yeye ni Mkuu wa Shule ya Insia na Sayansi ya Jamii katika Chuo Kikuu cha Pwani, Kilifi Kenya.

Chimera ameandika riwaya, na tamthilia zikiwemo kama vile; Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* (1995), *Siri Sirini* (2013/2014) na Tamthilia ya *Mnara Wawaka Moto* (1998). Vile vile Chimera ameandika vitabu vingine kadhaa kama vile: *Past, Present and Future Horizons* (1998).

## 3.0 Taswira ya Misri kwa Mujibu wa Riwaya Mbili Hizi

Upitiaji wa Riwaya mbili hizi ambazo data ya Makala haya imekusanywa ni wazi kuwa waandishi wawili hawa (Shafi na Chimera) wamechora taswira iliyo wazi na ya kiuhalisia ya Misri kupitia ufuatiliaji wao wa mipaka na ufafanuzi wao wa mambo ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na maisha kwa jumla kama ifuatavyo:

### 3.1 Miji ya Misri

Waandishi wawili hawa wameweza kuielezea miji ya Kimisri kwa njia ya kweli na sahihi kwa mtindo wa fasihi fasaha katika riwaya zao, miji hiyo ni pamoja na Cairo, Giza, Alexandria, Port Said, na Misri ya Juu.

### 3.1.1 Miji ya Misri Kwa Mtazamo wa Chimera

Katika Riwaya ya *Siri Sirini*, Mfalme wa Shanga alipeleka ujumbe rasmi kwenda Misri. Ujumbe huu ulikuwa na watu wanne ambao ni Waziri Mkuu, Mshauri Mkuu wa Mfalme, Mwanafaume, na Waziri wa Mambo ya Nje. Ujumbe huu ulipanda meli kutoka Shanga, ambayo ilikuwa katika kisiwa cha Pate wakati huo, hadi kufikia Kisiwa cha Lamu. Kutoka hapo walipanda meli ya kimisri iliyokuwa ikiwasubiri na kusafiri nayo katika Bahari ya Hindi, wakapitia Bahari Nyekundu hadi wakafika Misri. Walipokanyaga tu nchi ya Misri walipokelewa na ujumbe wa ngazi ya juu wa Misri ulioambatana na msafara wa ngamia wanne uliowapitisha jangwani hadi Cairo. Baadae, Chimera alielezea miji ya Misri ambayo ujumbe wa Shanga uliona wakati wa ziara hii rasmi nchini Misri. Miji hii ni pamoja na Cairo, Giza, na Alexandria.

#### 3.1.1.1 Mji wa Cairo:

Mara tu wajumbe wa Shanga walipofika Cairo, walishangazwa na kile walichokiona, kama alivyosema Chimera:

“Waliona barabara pana, si vile vichororo vya kwao, vijibarabara vya punda na mikokoteni!” (Chimera 2013: 248)

Baada ya kumalizika kwa kikao cha kwanza cha mkutano wa ujumbe wa Shanga na wa Misri, ilikuwa ndani ya mpango wa ziara hiyo ya ujumbe huo ni kutembelea mji wa Cairo, kwa hivyo Chimera alielezea mshangao wa Mwanafaume wa Shanga kwa kile alichoona wakati huo, akisema:

“Aliziangalia barabara za Kahra (Cairo) akazia jinsi zilivyokuwa pana, ndefu na zisizopindapinda ovyo... Si hivyo tu, bali barabara zenyewe zilikuwa si za kifusi kama barabara za kwao zilivyokuwa. Hizi za Kahra zilikuwa zimejengwa maridadi kwa mawe ya chokaa yaliyopondwapondwa na kugandwagandwa yakageuka kuwa saruji maridadi. Kwa jinsi hii mji mzima ulikuwa hauna vumbi ijapokuwa barabara zenyewe zilijaa charioti nyingi wakati wote.” (Chimera 2013: 283)

Inafahamika kuwa mandhari ya kwanza ambayo ilivutia ujumbe wa Shanga na kuwashangaza ni upana wa barabara za Cairo, upangaji wake mzuri na uzuri wa lami yake, ambayo inaoneha kiwango cha maendeleo ya Misri katika kipindi hiki ambacho Chimera anakizungumzia. Kipindi hicho labda kilikuwa ni cha mwishoni mwa karne ya kumi au wakati wa karne ya kumi na moja BK.

#### 3.1.1.2 Mto wa Nile:

Mto wa Nile ni moja ya alama muhimu zaidi za Misri ambazo huvutia wageni, na kwa hivyo, ujumbe wa Shanga ulivutiwa na Mto wa Nile vilevile kama Chimera alivyosema:

Waliona mto Nili (Nile), Nili kweli, samawati ya mbingu, mpana uliozagaa pengine pengine jijini Kahra, merikebu nyingi na majahazi, vyombo ashirafu, vikielea kwa maringo na madaha kama watu...! (Chimera 2013: 248, 249)

Wajumbe wa Shanga walivutiwa na Mto wa Nile, rangi yake ya kupendeza, na kupanuka kwake katikati mwa Cairo, na kushangaa kwao kuliongezeka kwa merikebu nyingi na majahazi yaliyokuwa yakielea humo. Chimera aliangalia madaha na maringo ambayo Wamisri walikuwa nayo, kwa hivyo alifananisha merikebu na majahazi yaliyopambwa na Wamisri katika maringo yao. Hii inaonesha uzuri wa merikebu hizi.

### **3.1.1.3 Ikulu ya Mfalme**

Chimera alielezea jinsi Mwanafaume wa Shanga alivyoshangaa alipoona Ikulu ya Mfalme huko Cairo, akasema:

“Hatimaye wakaliona gongwa la Mfalme wa Misri. We, baba we! Mwanafaume moyo ulimpiga pute, akaona aibu kujaribu kulinganisha magongwa ya babake na hili gome lililoshambuliwa macho yake bila mbwawazi! Si fahari hiyo! Si upambe huo! Si kivuta-nadhari hicho! Si anasa hizo!” (Chimera 2013: 249)

Moyo wa Mwanafaume ulimpiga pute akielezea mshangao wake kwa Ikulu ya Ufalme wa Misri na eneo lake ambalo ni kubwa mno. Aliona ni aibu kulinganisha kati ya majumba ya baba yake huko Shanga na jumba hili zur. Alitumia neno la ‘Gome’ kumaanisha kasri kubwa mno, na neno hili linaonesha ukubwa wa jumba hilo.

### **3.1.1.4 Bustani ya Ikulu ya Mfalme**

Mkutano wa kwanza kati ya wajumbe wa Shanga na wa Misri ulifanyika katika bustani kubwa iliyounganishwa na Ikulu ya Mfalme huko Cairo. na Chimera alielezea bustani hii, maua yake, matunda yake na ndege wake walioashiria jinsi Wamisri walivyosherehekea wajumbe wa Shanga, kwa kusema:

Bustani yenyewe ilikuwa na maajabu mengi... Ilikuwa na maua ya aina aina tena ya kila rangi. Ndani ya bustani pia mlipatikana miti ya matunda waijuayo Washanga na mingi tu wasiojua...Fauka ya hayo, bustanini mlikuwa mmejaa ndege aina mbalimbali, wakubwa kwa wadogo, wakirukaruka mahali pote bila kuogopa wanadamu...katika sehemu fulani fulani, kulikuwa na vijito ambavyo vilikuwa vikitiririka daima... Vile vile maji yalitoka na kutiririka katika vinywa vya vichwa vya simba wa kutengenezwa kwa mikono ya watu... Nyuma ya simba hao miale ya jua iliweza kupenya na kuimulika michirizi hiyo ya mvua daima dawamu. (Chimera 2013: 273, 274)

Sio hivyo tu, lakini Chimera alielezea magofu yaliyokuwepo katika bustani hii ambayo yanajumuisha historia ya Misri, kwa kusema:

“Sanamu hizo, kwa kuziangalia tu, zilieleza mapisi yote ya Misri kongwe. Baadhi ya sanamu zilizokuwamo ni kama vile za mafarao Ramesisi wa kwanza na wa pili, Amen Hotep, mkewe Malkia Nefrititi, Tutankhamon, Malkia Hatshepsut na hata watawala wa



zama za majuzijuzi kama vile Khalikizanda Mtukuka na Malkia Kliopatra.” (Chimera 2013: 274)

Yeyote anayechunguza bustani hii ambayo mkutano ulifanyika anaona kwamba uchaguzi wake haukuwa wa kubahatisha, bali ni chaguo bora na linalofaa kwa tukio hilo. Maua yake anuwai katika rangi zake yalionesha furaha na shangwe iliyosheheni mkutano huu wa kindugu, na matunda yake mengi ambayo watu wa Shanga wanayajua mengine na hawajui mengi ni ishara ya ukarimu na ukaribisho mzuri kutoka Serikali ya Misri kwa wajumbe wa Shanga. Ndege wengi ambao walikuwa wakirukaruka huku na huko bila kuogopa, ni ishara ya usalama, amani na utulivu uliokuwepo kote Misri. Maji yake yaliyotiririka kutoka vinywani mwa simba na ambayo miale ya jua iliweza kupenya na kuimulika michirizi hiyo ya mvua, ni ishara ya kuongezeka kwa uzuri kwenye kikao hicho.

Kuhusu kuwepo magofu ya kimisri, katika mahali hapo kunakumbusha uhalisia, utukufu wa ustaarabu wa Wamisri, ambao ni mmoja miongoni mwa ustaarabu wa zamani zaidi ulimwenguni. Kwa hivyo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Shanga aliongozwa na mambo haya ya kale ya Misri na kutokana na kile alichona mahali pale alisema katika hotuba yake aliyoitoa kwa hadhira, akisisitiza kwamba:

“Misri ni ulimwengu nao ulimwengu ni Misri.” (Chimera 2013: 277)

Na kwamba bila Misri, wanadamu wangukuwa wana tofauti ndogo sana na mahayawani. Na kwamba Misri ndio iliyowafunza wanadamu kuwa watu, kuwa na utu, na hivyo basi kuepukana na unyama. Na kwamba ustaarabu wote ujulikanao leo chimbuko lake ni nchini Misri. Misri ni nchi ya manabii kama vile; Nabii Yusuf, Nabii Musa, Nabii Issa, na Nabii Muhammad, A.S. ambao wote walifika Misri. Dini ya Kikristo ilianza Misri na kupata mashiko makubwa tangu awali kabisa. Kanisa la kale kabisa ulimwenguni liliasisiwa huko Misri, ambalo si jengine bali ni Kanisa la Kikoputi. Na kwamba uhusiano baina ya Misri na Barazinji una mapisi marefu, tena marefu sana. Uhusiano huu ulianza enzi ya utawala wa Malkia wa Hatshepsut uliokuwa baina ya 1490 na 1469 kabla ya Nabii Issa kuzaliwa. Ambapo kulikuwa na uhusiano wa kibiashara kati ya Misri na Barazinji, ambayo iliitwa Punt inayotamkwa ‘Pwani’, katika ulimi wetu wa Kiswahili hadi leo. (Chimera 2013: 277-280).

Kutokana na maneno ya hapo juu yaliyotajwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Shanga inaonekana kwamba baadhi ya ukweli wa kihistoria aliotaja ni sahihi na mwengine sio sahihi. (عبد الجواد Abd Al-Jawad 1984: 97) alithibitisha hoja ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Shanga kwamba Misri ni nchi ya manabii, kwa kusema: Ikiwa tunawafuata manabii waliofika Misri, tunapata kuwa baba wa Manabii Ibrahim, Yakobo, Musa na Issa, A.S., wote walifika Misri. Baadhi yao walikaa kwa miezi michache, kama baba wa Manabii Ibrahim, A.S., na wengine walikaa kwa miaka mingi hadi wakafa katika nchi ya Misri, kama vile Nabii Yakobo, A.S., ambaye alifika Misri akiwa na umri wa miaka 147, Issa, A.S., ambaye alikaa katika Misri kwa miaka 14 na mama yake; Bikira Maria. Naye Nabii Yusuf, A.S., alifika Misri akiwa na miaka 13 na akafa huko akiwa na miaka 110.



Kwa upande mwingine hakuna yeyote miongoni mwa walioandika Sira ya Nabii Muhammad, S.A.W., aliyetaja kwamba Nabii Muhammad alizuru Misri, kama Chimera alivyosema kupitia Waziri wa Mambo ya Nje wa Shanga. Kuhusu mwanzo wa kuibuka kwa dini ya Kikristo huko Misri, kulingana na شبيحة (Shiha 1988: 13) kwamba dini ya Kikristo ilifika hapo baada ya Familia moja Takatifu kukimbilia Misri mnamo mwaka wa kwanza BK kwa kuogopa kuteswa na watawala wa Palestina. Kanisa la Kikoputi ni moja ya makanisa ya zamani zaidi ulimwenguni, lililojengwa katika tarehe ya enzi ya Mitume ya Kwanza, ingawa hakuna nyaraka zinazolirejelea tarehe hii, kama hali ilivyo kwa makanisa ya kwanza ya Siria na Kirumi. Kupitia maneno haya, inakuwa wazi kuwa kanisa hilo sio kanisa la zamani kabisa ulimwenguni, kama Waziri wa Mambo ya Nje wa Shanga alivyosema.

Kuhusu Malkia Hatshepsut, (سليم Selim 1989: 148) anathibitisha kuwa malkia huyu alikuwa ameandika kwenye ukuta ambao unagawanya barabara kuu ya hekalu la Deir El-Bahari habari za safari yake iliyompeleka katika nchi ya Punt, na safari hiyo ilikuwa na meli tano kubwa, na meli hizi zilileta bidhaa za nchi hii kama vile; meno ya tembo, mpingo, kuni, ngozi za chui, za nyani, na pia zilileta miti ya uvumba ambayo ilisafirishwa na mizizi yake kwa kuhifadhiwa kwenye vikapu na sufuria za udongo. Chami (2002: 23) alielezea kuwa pwani ya Afrika Mashariki ilikuwa ni sehemu ya Punt, na akiolojia iliunga mkono maoni haya, ingawa baadhi ya wasomi walikuwa wakisema kwamba nchi za Punt ziko kwenye upande wa Kaskazini mwa Afrika, ambayo ni, Somalia na Ethiopia.

Ikiwa neno Punt lilitamkwa na Waswahili wa Pwani, kulingana na Chimera, basi hii inaweza kuonesha kuwa tangu enzi za kabla ya Ukristo, nchi hizi ziliitwa nchi za Pwani. Reusch (1961: 11) amesisitiza kuwa kuna utangamano katika matamshi kati ya maneno haya mawili (Punt na Pwani) kwa sababu matamshi katika lugha ya zamani ya Kimisri inaruhusu hivyo.

### 3.1.1.5 Mji wa Giza

Ratiba ya ziara ya ujumbe wa Shanga huko Misri ilionesha kuwa kulikuwa na ziara ya kutembelea katika maeneo ya Piramidi za Giza na Sphinx, na mara tu walipofika hapo, akili zao zilishangazwa na kuanza kuuliza maswali ambayo yalikuja akilini mwao kama ifuatavyo:

Jamani! Iliwezekanaje kulijenga jisanamu lile la kichwa cha mtu na mguu wa simba, jisanamu la aushi lililokula miaka kikwi kadhaa! Na hizi piramidi je? Si zilizengwa na Nabii Musa pamoja na Firauni hizi? Ni miaka mingapi kabla ya kuzaliwa Nabii Issa?! ... Waliona mizigo ya mawe yaliyotumiwa kuzijengea, miamba mikubwa kuliko kimo cha mtu! Na piramidi zenyewe zilikuwa ndefu, ndefu mno zikilekea mawinguni. (Chimera 2013: 290,291)

Wajumbe wa Shanga walisema kwamba Nabii Mussa na Firauni ndio waliojenga piramidi, habari ambayo si sahihi kwa sababu wajenzi wa piramidi - kama ilivyotajwa na (شبيحة Shiha, 1988: 58) – wanafuata familia ya nne katika Ufalme wa Kale. Hata hivyo, utafiti wa hivi karibuni umethibitisha

- kufuatana na ( عبد الجواد Abd Al-Jawad, 1984: 116) - kwamba Firauni wa Mussa ni Merneptah ibn Ramses II (katika familia ya kumi na tisa).

### 3.1.1.6 Mji wa Alexandria

Baada ya wajumbe wa Shanga kutembelea piramidi za Giza, ilipangwa - kulingana na Ratiba ya ziara - kusafiri kwenda Mji wa Alexandria, na mara tu walipofika, Chimera alisema:

“Wakakanyaga ardhi ya jiji la Khalikzandria. Wageni wakashtuka hadi walipobaini uzuri wa jiji hilo jinsi walivyoliona toka pale bandarini walipokuwa. Mwanamfaume alishangaa sana alipoona jiji lililorefuka kuambaana na bahari masafa marefu, marefu sana, kiasi mwisho wake ukamshinda kabisa kukadiria kutoka pale walipokuwa.” (Chimera 2013: 302)

Mara tu merikebu ilipotia nanga bandarini mwa Alexandria, wajumbe hawa wa Shanga walishangazwa na uzuri wa mji ule na kupanuliwa kwake kwenye pwani ya bahari ya Mediterania. Hii inaonesha uchawi wa mji huo ambao unavutia mioyo kabla ya macho. Kwa hivyo, (ابن حوقل Ibn Hawqal 1992: 141) alielezea, akisema: Ni mojawapo ya miji maarufu nchini Misri na una magofu ya ajabu. Ni mji ulio kwenye Bahari ya Rum. Michoro yake ni dhahiri, na athari za watu wake ni wazi sana. Una barabara zilizowekwa aina mbalimbali za mawe.

( Al-Qazwini الفزويني, Pasipo na Tarehe: 143) alisema kuhusu Alexandria: Ni mji maarufu wa Misri ulio kwenye pwani ya bahari. Wanahistoria wametofautiana kuhusu nani aliyeujenga: Wengine miongoni mwao walisema kwamba mji huo ulijengwa na Alexander wa kwanza, ambaye ni Dhu Al-Qarnayn, Ishak ibn Sulukoos Al-Rumi ... na wengine walisema kuwa ulijengwa na Alexander bin Dara, mwana wa binti wa mwanafalsafa wa Ar-Rumi.

Baada ya wajumbe hawa wa Shanga kushangazwa na mji wa Alexandria, Mwanamfaume wa Shanga alitaka kujua historia ya mji huo mkubwa. Waziri wa Mambo ya Nje wa Shanga alimjibu kuwa aliyeujenga ni Alexander Al-Akbar kabla ya kuzaliwa kwa Nabii Issa kwa miongo mitatu. Naye Alexander Al-Akbar wakati alipokuwa na umri wa miaka kumi na sita babake alikuwa amemwajiria mwalimu mkuu kabisa kuwahi kuishi siku hizo akiitwa Aristotoli, kutoka Uyunani. Na alipofikisha umri wa miaka kumi na minane, babake akampa cheo cha ujemadari, akamtuma aende akapambane na Uyunani. (Chimera 2013: 302-307).

### 3.1.2 Miji ya Misri Kwa Mtazamo wa Shafi

Shafi alipotembelea Misri mnamo 1961, alielezea maeneo ambayo alipitia, kuanzia kijiji cha Al-Shellal huko Misri ya Juu, wakati alipokuwa akija kwa treni kutoka hapo, akipitia Cairo, ambapo ndipo aliposafiria kwenda Port Said akiwa njiani kurudi Zanzibar.

#### 3.1.2.1 Misri ya Juu

Wakati Shafi alipopanda treni kutoka kijiji cha Al-Shellal, kusini mwa Aswan, akielekea Cairo, huku akipitia mikoa ya Misri ya juu, alisema:

“Tulipita kandokando ya mashamba yaliyostawi mimea vizuri kwa baraka ya maji ya Mto Nile... Mara mojamoya tuliwaona wakulima wakilima kwa majembe yaliyokuwa yakikokotwa na nyati. Treni ilipopita pempezoni mwa mashamba yao walitupungia mikono kutusalimu.” (Shafi 2013: 367).

Shafi alisafiri kwa treni kutoka kijiji cha Al-Shellal, akielekea Cairo, na pande zote za barabara hii kuna mashamba ambayo yanamwagiliwa kwa maji ya Mto wa Nile, kama Shafi alivyosema. Inaonekana kwamba treni ilikuwa ikienda asubuhi mapema, kwa hivyo Shafi aliwaona wakulima wakifanya kazi zao katika mashamba na mara tu walipoona treni waliwapungia mikono kuwasalimu abiria. Hii inaweza kuashiria tabia ya ukarimu ambao watu wengi wa Misri ya Juu wanayo.

### **3.1.2.2 Mji wa Cairo**

Mara tu Shafi alipofika Cairo, alishangazwa na kile alichokiona:

Tulitoka katika eneo la stesheni ya reli tukaingia ndani ya jiji la Kairo, jiji kubwa kuliko miji yote ya Afrika. Tuliliona jiji hilo jinsi lilivyokuwa limejaa shughuli. Watu walikuwa wamejaa barabarani, wengi kama siafu. Mabasi yalikuwa yamesheheni abiria mpaka wengine wakining'inia nje. Kwa mara ya kwanza niliziona treni zilizotembea barabarani, nazo zilikuwa zimesheheni abiria tele... (Shafi, 2013: 369, 370).

Shafi alionesha mwanzoni mwa riwaya yake kwamba alitembelea Cairo mnamo mwaka 1961 BK, na sio siri kwa mtu yeyote kwamba karibu miaka mitano kabla ya kipindi hiki, Misri ilishambuliwa na Vita vya 56, na ikapata hasara kubwa, pamoja na idadi ya watu, ambayo wakati huo ilizidi watu milioni 27. Kwa hivyo, hali ile ambayo Shafi aliiona ya idadi kubwa ya watu barabarani na msongamano mkubwa katika vyombo vya usafiri, ambayo inaweza kuonesha uhaba wavyombo vya usafiri wa umma wakati huo, na hali hii ni ya kawaida baada ya kipindi hiki kigumu na hali mbaya hiyo ambayo Misri ilipitia.

### **3.1.2.3 Midan El-Tahrir (Uwanja wa Uhuru)**

Wakati Shafi alipokuwa akielekea eneo la Zamalek, alipita karibu na uwanja wa Tahrir na kuuelezea, akisema:

“Hapo palikuwa “Midan-el-Tahrir” au uwanja wa uhuru. Ule mzunguko wa kuzunguka magari ulikuwa katikati ya njia kuu nne kila moja ikielekea upande wake. Upande wetu wa kulia kilikuwepo kituo cha treni za barabarani na watu waliokuwa wamejaa hapo tele waligombania kuingia katika kila treni iliyosimama hapo. Upande wetu wa kushoto lilikuwepo jengo kubwa ambalo baadaye tulikuja elewa kuwa humo zilikuwemo ofisi mbalimbali za serikali. Mbele yetu lilitusimamia pandikizi la nyumba, juu limebeba maandishi yaliyoandikwa “Nile Hilton”.” (Shafi 2013: 376)

Uwanja wa Tahrir ni moja ya alama za Misri na ndio uwanja mkubwa zaidi wa Cairo, kwani unaunganisha maeneo muhimu zaidi katikati yake, na wakati huo ilikuwapo tramu. Jengo ambalo lilikuwapo kushoto kwa Shafi ni jengo la huduma za serikali linalojulikana kama jengo la Mujamaa Al-Tahrir. Kuhusu nyumba kubwa iliyokuwapo mbele ya Shafi, ilikuwa moja ya hoteli za kifahari zaidi za Misri wakati ule, iliyoitwa Hoteli ya Nile Hilton.

#### **3.1.2.4 Daraja la Zamalek**

Miongoni mwa mambo ambayo yalimshangaza Shafi wakati wa ziara yake huko Cairo ni Daraja la Zamalek, ambalo alilielezea kwa kusema:

“Daraja la Zamalek lilikuwa limebebwa na mihimili ya zege zito na vyuma madhubuti. vilikuwa vimeshindiliwa kuanzia chini ya maji ya Mto Nile hadi juu ya lililotandikwa daraja hilo, kuanzia ng'ambo moja ya jiji la Kairo hadi ng'ambo nyingine.” (Shafi 2013: 380)

Daraja la Zamalek ni daraja linalounganisha eneo la Zamalek huko Giza na kitongoji cha Bulaq Abu Al-Ela huko Cairo. Daraja hili limesaidia kuongeza ujenzi wa eneo la Zamalek tangu 1912 (الطريبي Al-Tarabili, 1996: 165). Shafi alipopita karibu na Daraja la Zamalek, alishangazwa na ukubwa wa mihimili ya zege zito na vyuma vilivyokuwa vimewekwa kwenye daraja hili na kuanzia chini ya mto hadi juu, hali ambayo inaonesha kwamba huenda Shafi alikuwa hajawahi kuona daraja kama hilo hapo awali, na hii vile vile inaonesha kiwango cha maendeleo ya Misri wakati huo.

#### **3.1.2.5 Mto wa Nile:**

Shafi pia alishangazwa na Mto wa Nile wakati alipopita kwenye njia yake kwenda eneo la Zamalek, ambapo marafiki zake wengine walikuwa wakiishi hapo wakati huo, akisema:

“Hapo, mto ulikuwa ukielea taratibu kama kwamba ulikuwa umechoka sana baada ya safari ndefu ya kutokea Uganda. Mashua na merikebu zilikuwa zimeegesha pembezoni mwa mto huo na kuonesha mandhari ya bandari iliyokuwa barabarani.” (Shafi 2013: 378)

Shafi alipoangalia Mto wa Nile, alikumbuka umbali mrefu ambao mto huu ulikuwa umesafiri kutoka chanzo chake nchini Uganda hadi kufikia Cairo, na wakati huo huo Shafi alikumbuka safari yake ngumu ambayo ilikuwa ni kutoka Zanzibar hadi Cairo, kwa hivyo alifikiria kwamba mto ulikuwa umesumbuliwa na uchovu kwa sababu ya safari yake ndefu, kwa hivyo, unatembea polepole kwa sababu umechoka kama yeye mwenyewe.

#### **3.1.2.6 Hali ya Hewa katika Cairo:**

Shafi alielezea hali ya hewa wakati alipotembelea Cairo, kwa kusema:

“Kairo palikuwa na baridi ya kuburudisha na kuchangamsha. Ulikuwa msimu wa kipupwe.” (Shafi 2013: 375).

Labda Shafi alitembelea Cairo katika kipindi cha Desemba 1960 BK hadi Februari 1961 BK, kwani kipindi hiki ndicho cha msimu wa baridi huko Misri.

### 3.1.2.7 Mji wa Port Said

Shafi alilielezea eneo aliloliona kutoka kwenye dirisha la chumba alichokuwamo wakati akienda Port Said, kwa kusema:

“Nilipolivuta pazia la dirisha la chumba kile na kuangalia nje, niliona bahari ya Mediteranian kwa mbali imekoza rangi ya feruzi. Mapovu meupe ya mawimbi yalikuwa yakipwitapwita juu yake. Ilikuwa imetanda mpaka upeo wa macho, kule ilikokutana na mawingu ya zambarau yaliyojitokeza kuikaribisha asubuhi ya siku ile.” (Shafi 2013: 414, 415).

Shafi aliizungumzia mandhari ya Bahari ya Mediterania ambayo mji wa Port Said unaiangalia kutoka kaskazini, kwa kuielezea rangi yake ya zambarau iliyoakisiwa kutoka kwa rangi ya mawingu, na kuchanganywa kwake na rangi nyeupe inayoonekana kwa sababu ya mawimbi. Picha hii nzuri iliyooneshwa na mwandishi inaweza kuipatia hisia ya burudani, faraja, na utulivu.

## 3.2 Vipengele vya Kijamii Nchini Misri kwa Mujibu wa Data za Makala haya:

Shafi na Chimera walisawiri katika riwaya zao hali ya maisha ya kijamii, ya kiuchumi na ya kisiasa iliyokuwa imeenea nchini Misri katika kipindi cha kutukia matukio ya kila riwaya, kama ifuatavyo:

### 3.2.1 Vipengele vya Kijamii:

Waandishi wawili wameonesha kwamba Misri ina matabaka mbalimbali. Na kama tunavyojua kwamba tofauti hii ya matabaka ipo katika kila jamii duniani, sio katika Misri tu. Waandishi hawa wameashiria hivyo kupitia maelezo yao kwa mavazi ya Wamisri, na tabia zao.

#### 3.2.1.1 Mavazi Katika Riwaya ya *Siri Sirini*:

Mavazi katika enzi ya Kifatimi huko Misri yalionesha tabaka la mtu binafsi ambalo ni mali yake. Kwa hivyo, Chimera anaelezea katika riwaya yake mavazi ya wanawake, ya wanaume na ya madereva wa vibandawazi vya kukokotwa na mafarasi ambavyo wajumbe wa Shanga walivipanda mara tu walipofika pembezoni mwa Cairo.

##### 3.2.1.1.1 Mavazi ya Wanawake:

Chimera aliyaelezea mavazi ya wanawake katika riwaya yake kwa kusema:

“Wanawake ambao walikuwa wamevaa mavazi yaliyovifunika viwiliwili vyao gubigubi isipokuwa macho tu... Wanawake wengine walikuwa wana mapambo vichwani na mabegani kama yale yaliyoonekana kwenye picha za Malkia wa kale Nefrititi.” (Chimera 2013: 327)

Chimera aliashiria mavazi ya matabaka mawili ya wanawake waliohudhuria karamu ya kuaga iliyoandaliwa na Mfalme wa Misri wakati huo kwa wajumbe wa Shanga, akisema kwamba tabaka la kwanza linaweza kuwa tabaka la kawaida la wanawake, kwani wamevaa mavazi ambayo yanafunika mwili mzima isipokuwa macho tu, na kufuatana na أحمد Ahmad (1993: 154-157) alisema kuwa: Mwanamke katika enzi ya Kifatimi mara nyingi alikuwa akivaa vazi refu lililofikia mguu, na wakati mwingine lilikuwa refu sana.. Mwanamke alijua nikabu katika enzi ya Kifatimi na haikuwa vazi la

mwanamke aliye Mwislamu tu, lakini ilikuwa pia vazi la mwanamke asiye Mwislamu, kwa hivyo lilifunika uso isipokuwa macho tu.

Kwa upande wa tabaka la pili la wanawake, wao walikuwa wamevaa mapambo vichwani na mabegani, kama Malkia Nefertiti alivyokuwa akivaa. Mapambo hayo yanaitwa taji kama ilivyoenezwa na أحمد Ahmad (1993: 151), nayo ni aina ya kifuniko cha kichwa ambacho wanawake walikuwa wakivaa enzi ya Kifatimi, nayo ni kama kofia ya juu ambayo ilikuwa na lulu na vito, na taji hili ni maalumu kwa wanawake wa tabaka tawala na tabaka la kiungwana katika jamii.

### 3.2.1.1.2 Mavazi ya Wanaume:

Kuhusu mavazi ya wanaume Wamisri waliokuwa wakipokea wajumbe wa Shanga, Chimera aliyaelezea mavazi yao kwa kusema:

“Watu hao walikuwa wamevalia mavazi ashirafu ajabu, mavazi yaliyompendeza kila mwenye kumbonekeza. Kuwatazama tu, wageni wakaamua kuwa wenyeji hao ni baadhi ya waungwana wa Misri wa tabaka la juu.” (Chimera 2013: 245)

Chimera alieleza mavazi ya wanaume ambao walikuwa wakipokea wajumbe wa Shanga baada ya kuwasili Misri kwamba walikuwa waungwana wa Misri wa tabaka la juu kutokana na mavazi yao ya kushangaza, ya kifahari. الأحمر Al-Ahmar (2012: 220) aliyaashiria mavazi ya viongozi wa serikali katika enzi ya Kifatimi, akisema: mavazi ya wakuu na viongozi yalisukwa kutokana na vitambaa vilivyopambwa, na wakuu walitofautishwa na wengine kwa kuvaa mkufu wa kitambaa kilichopambwa, na kuwekwa shingoni, unaoitwa "kola" ... Wakuu kwa ujumla walivaa vilemba vilivyotengenezwa kwa kitambaa kilichopambwa kwa dhahabu na kupambwa kwa vipande vidogo vidogo vya chuma cha dhahabu au cha fedha.

Inafahamika kuwa maelezo yaliyotolewa na Chimera kuhusu mavazi ya wanaume hawa na kwamba walikuwa wamevaa mavazi ya waheshimiwa yanaonesha kabisa kile الأحمر Al-Ahmar alichoashiria kuhusu mavazi ya wakuu na viongozi, na pia kuwepo kwa mfumo wa tabaka katika Jamii ya Wamisri wakati huo.

### 3.2.1.1.3 Mavazi ya Madereva wa Vibandawazi:

Kuhusu mavazi ya madereva wa vibandawazi ambao wajumbe wa Shanga walivipanda walipofika Cairo, Chimera aliyaelezea kama ifuatavyo:

“Walikuwa hawakuvaa libasi zozote kutoka kiunoni kwenda juu, shingoni walikuwa wamevalia mapambo mapambo kabisa yaliyoshukia chini na kuziba vifua vyao na mabega. Kutoka viunoni walikuwa wamevaa aina ya saroni zilizokuwa maridadi sana.” (Chimera 2013: 248)

Maelezo yaliyotajwa na Chimera kuhusu mavazi ya madereva wa vibandawazi yanafanana sana na maelezo ya mavazi ya askari wa kijeshi waliofuata Ufalme wa Misri wakati huo. ماجد Majid (1955: 59) alitaja mavazi ambayo yaliwapambanua askari hawa kwa kusema kwamba walivaa mavazi maalumu na walikuwa wakitembea kwa gwaride la kifalme na ngao. إبراهيم Ibrahim (2007: 104)

alisema kuwa yalienea katika enzi ya Kifatimi mashati ya chuma yaliyovaliwa mwilini na yenye mikono mifupi ambayo ni mavazi ya askari na mashujaa.

Msomaji akifikiria kile Chimera alichoelezea kuhusu mapambo ambayo yalivaliwa shingoni, yaliyoshukia chini na kuziba vifua na mabega, ataelewa kuwa hizo ni ngao ambazo ماجد Majid alizitaja, au huenda ni mashati ya chuma ambayo إبراهيم Ibrahim alikuwa akiyazungumzia katika ufafanuzi wake wa mavazi ya askari na mashujaa katika enzi ya Kifatimi.

### 3.2.1.2 Mavazi Katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani:

Shafi aliyaelezea mavazi ya Wamisri aliowaona kwenye mashamba ya Misri ya Juu, kwa kusema:

“Pale Shellal tulianza kuona dalili za kuwa tumeshaingia Misri kutokana na libasi ya watu wa hapo. Wanaume ndani ya makanzu mapana bwangabwanga na tarbushi kichwani, wanawake ndani ya mabuibui meusi.” (Shafi 2013: 367).

Katika miaka ya sitini ya karne ya ishirini, kulikuwa na baadhi ya Wamisri, haswa katika mashamba ya Misri ya juu, ambao walikuwa bado wakivaa makanzu na tarbushi kichwani. إبراهيم Ibrahim (2002: 299) alisema kwamba tarbushi iliyokuwa ikivaliwa kichwani ilikuwa ikitumika kuanzia mwanzoni mwa enzi ya kisasa (kuanzia mwaka wa 1805) huko Sham, Misri na Moroko.

Wanawake huko Misri ya Juu wakati huo walikuwa wakivaa mabuibui meusi. علماء الحملة الفرنسية. Wasomi wa Kampeni ya Ufaransa (1993: 116) walisema kwamba wanawake wa shamba walikuwa wakivaa tu suruali na shati pana sana juu yake, lenye mikono mirefu na mipana lililoshuka hadi kwenye makalio.

### 3.2.1.3 Tabia za Wamisri Katika Riwaya Mbali

Katika riwaya zao, Shafi na Chimera walizielezea tabia za Wamisri kuwa ni za madaha na maringo. Katika riwaya ya *Siri Sirini*, wajumbe wa Shanga walipoona merikebu na majahazi yakisafiri kwenye Mto wa Nile waliileza taswira hiyo kwa kusema:

“Merikebu nyingi na majahazi, vyombo ashirafu, vikielea kwa maringo na madaha kama watu...!” (Chimera 2013: 248, 249)

Chimera alifananisha merikebu na majahazi na watu katika maringo yao. Kuhusu riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, wakati Shafi na rafiki yake Abdullah walipokuwa wakiuliza watu kuhusu eneo la Zamalek, wakapuuza, kwa hivyo Shafi akamwambia Abdullah:

“Si nilikwambia kuwa tumefika nchi ya Firauni? ... Firauni alikuwa anajiona ni yeye tu, hakuna mwingine kama yeye, na watu wa nchi hii wamerithi tabia hiyo.” (Shafi 2013: 375).

Kupitia maneno ya Chimera na Shafi, imebainika kuwa waandishi wote wawili waliwaelezea Wamisri kwa ujumla kuwa wana tabia za maringo na kiburi. Huu ni uamuzi wao wa jumla, na sio sahihi kutoa uamuzi wa jumla kwa wanajamii wote. Kwa sababu kila jamii ina wazuri na wabaya wake, kwa hivyo, uamuzi huu wa jumla hauna uadilifu.



### 3.2.2 Vipengele vya Kiuchumi:

Katika riwaya ya *Siri Sirini* Chimera ameashiria kiwango cha juu cha uchumi wa Misri. Lakini katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* Shafi ameashiria kwamba kiwango cha uchumi wa Misri wakati ule kiliongezeka. Waandishi wawili walitaja vipengele vya kiuchumi nchini Misri kupitia vyombo vya usafiri vilivyotumika wakati huo, na kiwango cha uchumi cha wanajamii wa kimisri. Aidha, Shafi pia alizungumzia kiwango kikubwa cha idadi ya masoko ya kibiashara katika mitaa ya Munira, kama ifuatavyo:

#### 3.2.2.1 Vyombo vya Usafiri wa Misri Katika Riwaya ya *Siri Sirini*:

Vyombo vya usafiri vinavyopatikana katika riwaya ya *Siri Sirini* vilikuwa ngamia ambao wajumbe wa Shanga waliwapanda mara tu walipofika nchini Misri, vibandawazi ambavyo walivipanda walipowasili Cairo, na jahazi ambayo waliisafiria kutoka Lamu kwenda Misri.

##### 3.2.2.1.1 Ngamia:

Waarabu walimwita ngamia jina la meli ya jangwani, kwa sababu wanasafiri umbali wa km 330 kwa mwendo wa kuendelea mchana, na kwa hivyo huzidi mara tatu ya njia ya farasi, na hubeba mgongoni mzigo wa kilo 200 (مقداد Miqdad, 2008: 262). Kwa hivyo, ngamia walitumika huko Misri enzi ya Kifatimi kama chombo cha usafiri kwenye barabara za jangwani. Wakati wajumbe wa Shanga walipofika mpakani mwa Misri kupitia Bahari Nyekundu, walikuta ngamia wanne wakiwasubiri ili wawafikishe Cairo. Chimera aliwaelezea ngamia hawa na wapandaji wao kwa kusema:

“Palikuwapo na ngamia wanne ambao walikuwa wametandikwa matandiko bora zaidi kuliko yale ya ngamia wa wenyeji. Ngamia hao wanne walikuwa na wapanzi ambao hawakuonekana kuwa ni waungwana kulingana na libasi zao.” (Chimera 2013: 246)

Chimera alitaja kwamba ngamia wametandikwa matandiko bora, na ماجد Majid (1955: 78,79) alionesha kwamba matandiko hayo yaliitwa عماريات Ammariyat, ambayo yalikuwa na mapazia ya hariri nyekundu, au manjano, yaliyofunikwa, kwa "hariri" na mikanda ya ngozi iliyotariziwa kwa fedha.

Kwa upande wa wapanda ngamia, hawa, ni miongoni mwa maofisa wadogo katika Serikali ya Kifatimi. الأحمر Al-Ahmar (2012: 220) aliashiria mavazi yao, kwa kusema: Kuhusu maofisa wadogo, mavazi yao yalikuwa ya bei rahisi, ambayo yana vipande viwili tu, shati na suruali, na mara nyingi yalitengenezwa kwa sufi na hariri. Hali hii ndio kama Chimera alivyoitaja kuhusu mavazi ya wapanda ngamia hawa, ambapo alisema kwamba mavazi yao, yakilinganishwa na mavazi ya waungwana, hawakuonekana kuwa miongoni mwao.

##### 3.2.2.1.2 Farasi:

Waarabu wanahusishwa na upandaji wa farasi, nao wamekuwa maarufu tangu nyakati za mwanzo katika historia ya kuhifadhi farasi na ukoo wao na sio kuwachanganya uzao wake (عشوب Ashoub, 2013: 29). Katika enzi ya Kifatimi, farasi walitumiwa kama chombo cha usafiri wa ndani. Kwa hivyo wakati wajumbe wa Shanga walipofika kwenye mipaka ya Cairo, walipokelewa na vibandawazi. Chimera alivutiwa na kuona farasi hawa, kwa hivyo aliwaelezea akisema:

“Jamani, farasi walikuwa wanapendeza we! Mbona walikuwa wameoshwa! Mbona manyoya yao yalikuwa yamelala maridadi na kuonekana laini mno, yenye kumetameta kama yaliyopakwa mafuta!” (Chimera 2013: 248)

wajumbe wa Shanga walishangazwa na uzuri wa mandhari ya farasi ambao waliwapokea tangu kuwasili kwao mipaka ya Cairo, na kwa kuongezea uzuri wa mandhari hiyo, ماجد Majid (1955: 22) alitaja kwamba matandiko ya farasi yalipambwa kwa nakshi, shanga kwenye shingo za farasi, na makalio ya nyuma na mbele ya ngamia yalijaa vito vya hali ya juu. Na hatamu zao zilikolezwa dhahabu na fedha.

### **3.2.2.1.3 Vibandawazi:**

Kuhsu vibandawazi ambavyo wajumbe wa Shanga walivipanda Cairo, Chimera alivielezea kwa kusema:

“Na charioti je? Gari nadhifu zenye magurudumu ya chuma zilizo na uwezo wa kwenda kasi kama vimondo, katika ardhi kavu!” (Chimera 2013: 248)

Chimera alielezea mshangao mkubwa wa wajumbe wa Shanga wakati walipopanda vibandawazi vilivyokuwa vimekokotwa na farasi wazuri, ambavyo viliwapokea wajumbe walipofikia mipaka ya Cairo. Vibandawazi hivi vilikuwa safi sana, na vilikuwa na magurudumu ya chuma yakisafiri haraka haraka.

### **3.2.2.1.4 Merikebu**

Wajumbe wa Shanga waliipanda merikebu kutoka nchini kwao kwenda bandari ya Kisiwa cha Lamu nchini Kenya kwa kuvuka Bahari ya Hindi, kisha wakapanda merikebu ya Kimisri kutoka Lamu mpaka Misri kupitia Bahari ya Mediterania. Chimera alielezea safari ya kutoka Lamu kwenda Misri kwa kusema:

“Safari ya kuelekea Misri ilikuwa tofauti katika kila namna... Safari yenyewe ilikuwa shwari kabisa na ya kupendeza.” (Chimera 2013: 244, 245)

Hali hii inaweza kuonesha kiwango cha maendeleo ya teknolojia ya ujenzi wa merikebu huko Misri wakati wa enzi ya Kifatimi, na hii ilithibitishwa na maelezo ya Chimera kuhusu merikebu ambayo wajumbe wa Shanga waliipanda walipokuwa wakienda Alexandria kwa kusema:

“Mfalme wa Misri aliwapa wageni wake merikebu yake binafsi: ‘Merikebu ya Mfalme’. Chombo hiki kilikuwa anasa tupu, kizuri upeo wa fani. Juu ya hivyo, kilikuwa kimepambwa kupindukia kama kwamba Mfalme mwenyewe alikuwa safarini.” (Chimera 2013: 301)

زكي Zaki (1966: 39) alisisitiza uzuri wa mandhari ya merikebu zilizomilikiwa na Mfalme wa Misri wakati huo, akiwasilisha maneno ya msafiri ناصر خسرو Nasir Khisru, kwa kusema: “Sultan alikuwa na merikebu ishirini na moja... kila moja ilikuwa na urefu wa dhiraa hamsini na upana wake ni dhiraa ishirini, imepambwa kwa dhahabu, fedha, vito na hariri”. Hii inaonesha kiwango cha anasa cha Mfalme wa Misri aliyeishi wakati huo.

### **3.2.2.2 Vyombo vya Usafiri wa Misri Katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani:**

Vyombo vya usafiri vilivyotumika katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* vilikuwa ni treni ambayo Shafi aliipanda kutoka kijiji cha Al-Shellal kusini mwa Aswan akielekea Cairo, teksi aliyoipanda kutoka stesheni ya reli hadi eneo la Zamalek, na gari alilopanda kwenda kambi ya kijeshi iliyopo katikati ya jangwa la Giza.

#### **3.2.2.2.1 Treni:**

Shafi alielezea treni aliyopanda kutoka kijiji cha Al-Shellal huko Misri ya juu akielekea stesheni ya reli huko Cairo, kwa kusema:

“Ndani ya treni viti havikuwa vya kugombania kama ilivyokuwa ndani ya treni tuliyosafiri nayo kutoka Khartoum hadi Wadi Halfa... Tuliingia katika behewa na tulilikuta tayari limejaa. Tulikimbilia behewa jingine, nalo lilikuwa tayari limejaa. Tuliendelea na kuelekea katika behewa la mbele zaidi. Hilo tulilikuta bado lilikuwa na mapengo mapengo ya viti vitupu.” (Shafi 2013: 367).

Treni hiyo ilikuwa ni chombo cha usafiri kilicho salama na cha haraka, ikiunganisha maeneo mengi, na Shafi alikuwa ameipanda treni hii kutoka stesheni ya reli kutoka kijiji cha Al-Shellal, kusini mwa Aswan, akielekea Cairo.

#### **3.2.2.2.2 Teksi:**

Teksi imetumika kama chombo cha usafiri wa ndani ya miji huko Misri. Shafi aliipanda teksi kutoka stesheni ya reli baada ya kuwasili Cairo, ambapo teksi zilisongamana. Kila dereva alitaka Shafi apande naye, kwa hivyo aliipanda moja ya teksi hizo akielekea eneo la Zamalek:

“Tuliingia ndani ya moja ya teksi hizo na tulimtaja dereva anuani ya pale tulipotaka kwenda Zamalek, Barabara ya Ahmed Hishmet, nyumba nambari Kumi na Tano. Dereva aliirekebisha mita ya kuhesabu pesa na safari ilianza.” (Shafi 2013: 369).

Inaeleweka kupitia maneno ya Shafi kwamba teksi zilikuwa nyingi na zinapatikana, Na hii inaonesha wingi wa usafiri wa kibinafsi huko Misri wakati huo, na labda hii ilisaidia - kwa kiwango fulani - kuondoa msongamano wa watu kwenye vyombo vya usafiri wa umma.

#### **3.2.2.2.3 Gari:**

Shafi alielezea gari alilopanda kwenda kwenye kambi ya kijeshi, kwa kusema:

“Gari lililokuja kutuchukua lilikuwa ni mkweche uliochoka kazi. Liliposimama mbele yetu breki zake zilikwaruzana kama zilizokuwa zikipigwa tupa. Lilisimama likayumba mbele na nyuma, halafu lilitulia huku likihema na kutoa moshi. Tuliingia humo mmoja mmoja. Gari lilikuwa na nafasi tele na tuliokuwemo humo tulipwaya ndani yake.” (Shafi 2013: 389).

Inaonekana kuwa vyombo vya usafiri ambavyo Shafi alivitaja katika riwaya yake, kuanzia treni, teksi na gari, vyote vilikuwa vyombo vya usafiri vya kisasa wakati huo na vilitumika wakati wa karne ya ishirini huko Misri.

#### **3.2.2.2.4 Tramu:**

Tramu ilikuwa moja ya vyombo vya usafiri vilivyotumika katika Cairo wakati wa karne ya ishirini, wakati treni zake zilipoanza kuendeshwa katika barabara za mji mkuu mnamo Agosti 12, 1897, kulingana na كيلاني Kilani (2010: 5). Shafi alisema kuwa aliona tramu ikiendeshwa kwenye barabara za Cairo:

“Kwa mara ya kwanza nilizona treni zilizotembea barabarani”. (Shafi 2013:370)

Hii inaweza kuonesha kiwango cha maendeleo ya Misri wakati huo katika uwanja wa usafiri, ingawa hasara zilizosababishwa na vita, ambavyo bado Misri ilikuwa inateseka na athari zake mpaka wakati ule.

### **3.2.2.3 Kiwango cha Uchumi wa Misri Katika Riwaya ya Siri Sirini:**

Chimera aliashiria kiwango cha uchumi wa Misri katika hotuba rasmi iliyotolewa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Shanga kwa Mfalme wa Misri wakati huo, akisema:

“Leo hii mashamba ya Misri yanazalisha vyakula vya kila aina, na hali hiyo imelifanya taifa hili kujitegemea siku zote.” (Chimera 2013: 278)

Kupitia dondoo hili, inafahamika kuwa Misri ilikuwa ikizalisha mazao mengi ya kilimo wakati huo, ambayo yaliifanya ijitosheleze, kama Chimera alivyosema. قلا Qula (2007: 34) aliashiria hivyo hivyo kwa kusema: Kilimo huko Misri kilijipambanua kwamba kilikuwa kikifikia kujitosheleza kwa wanajamii, siyo hivyo tu, bali Misri ilisambaza kwenye Misikiti Mitakatifu (Saudi Arabia) nafaka na maharagwe. Hii inathibitisha kiwango cha juu cha uchumi huko Misri wakati wa enzi ya Kifatimi.

### **3.2.2.4 Kiwango cha Uchumi wa Misri Katika Riwaya ya Mbali na Nyumbani:**

Shafi alielezea eneo la Zamalek na wakaazi wake, kwa kusema:

“Zamalek ni kisiwa kilichozungukwa na Mto Nile. Ni eneo waliloishi mabwanyenye na watu waliokuwa na uluwa na utukufu.” (Shafi 2013: 374).

بركة Barakah (2009: 147) alisisitiza hayo wakati alipojumuisha eneo la Zamalek kati ya vitongoji vya tabaka la juu, na akasema: Mnamo mwaka wa 1947, Zamalek ilikuwa na watu 65,000 waliotambulika kijamii ambao waliwakilisha sehemu kubwa ya “Tabaka la Juu.” Wakati Shafi alipoeleza eneo la Munira, alisema:

“Tuliamishiwa katika nyumba nyingine iliyokuwepo mtaa wa Munira, mbali kidogo na Zamalek” (Shafi 2013: 373).

Kisha akielezea barabara za eneo hili akisema:

“Tulikuwa tukikata kona za mitaa ya ndanindani iliyokuwa imejaa wachuuzi na maduka ya rejareja” (Shafi 2013: 375).

Kupitia yaliyotangulia hapo juu, inafahamika kuwa Shafi alikuwa akilinganisha kati ya kiwango cha uchumi cha wakaazi wa eneo la Zamalek na wale wa eneo la Munira, akielezea kuwa eneo la Zamalek limezungukwa na Mto wa Nile pande zake zote, na sehemu kubwa ya wakazi wake ni wa tabaka la juu. Kuhusu eneo la Munira, ambalo liko mbali kidogo na Zamalek, ni eneo lililojaa wauzaji na maduka ya rejareja, hali ambayo inaonesha kiwango cha chini cha uchumi cha wakaazi wa eneo hili. Hii inaweza kuonesha tofauti kati ya tabaka za jamii ya Wamisri wakati huo. Lakini utofauti huu upo katika kila jamii ulimwenguni, sio huko Misri tu.

### 3.2.2.5 Masoko Katika Riwaya ya *Mbali na Nyumbani*:

Wakati Shafi alipokuwa akielekea barabara ya Ahmed Heshmat huko Zamalek, alipita karibu na uwanja wa Al-Tahrir na kuelezea kama ifuatavyo:

“Kwenye uwanja huo walikuwepo watu waliokuwa na kila aina ya biashara ndogondogo. Vilikuwepo vibanda vidogo vidogo vya kuuzia vinywaji baridi. Wauza mikate walikuwa wamebeba masusu yaliyokuwa yamejaa mikate ya “Eish Balad.” Wasafisha viatu walikuwa wakiranda na vibao vyao na kumwania kila waliyemwona na kumlazimisha wamsafishie viatu.” (Shafi 2013: 376, 377)

Uwanja wa Al-Tahrir wakati huo ulikuwa umejaa vibanda vidogovidogo vya kuuzia kila aina ya biashara, na hii inaweza kuonesha kuongezeka kwa shughuli za kibiashara, wingi wa bidhaa mbalimbali, na mwanzo wa urejesho wa uchumi wa Misri baada ya kipindi cha vita cha 1956.

### 3.2.3 Vipengele vya Kisiasa kwa Mujibu wa Data za Makala haya:

Katika riwaya ya *Siri Sirini* Chimera ameashira kwamba katika wakati ule mfumo wa kisiasa nchini Misri ulikuwa wa kifalme. Lakini katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* Shafi ameashiria kwamba katika kipindi cha ziara yake kwa Misri mfumo wa kisiasa huko ulikuwa wa jamhuri chini ya uongozi wa Marehemu Rais Gamal Abdel Nasser. Waandishi wawili hawa wameelezea vipengele vya kisiasa huko Misri wakati wa kutukia kwa riwaya zao kama ifuatavyo:

#### 3.2.3.1 Vipengele vya Kisiasa Katika Misri Kupitia Riwaya ya *Siri Sirini*:

Matukio ya riwaya ya *Siri Sirini* yametukia mwishoni mwa karne ya kumi au mwanzoni mwa karne ya kumi na moja BK, kwani mmoja wa wahusika wakuu katika riwaya hii ni Fumo Liyongo, na kwamba Levtzion na Pouwels (2000: 524) na Harrow (1991: 38) wameonesha kwamba Fumo Liyongo aliishi Shanga chini ya utawala wa Mfalme Daudi Mringwari, wakati wa karne ya kumi BK. Mulokozi na Sengo (1995: 49) walisema kuwa Fumo Liyongo aliishi wakati wa karne ya tisa hadi karne ya kumi na mbili BK. Chimera alitaja katika riwaya yake kwamba Waziri wa Mambo ya Nje wa Shanga, ambaye alitembelea Misri na alikuwa miongoni mwa wajumbe wa Shanga, alikwenda Misri mara ya kwanza wakati alipokuwa akisoma katika Chuo Kikuu cha Al-Azhar, na inajulikana kuwa Chuo Kikuu cha Al-Azhar kilianzishwa mnamo 972 BK; Hiyo ni katika nusu ya pili ya karne ya kumi BK. Kwa hivyo wajumbe wa Shanga walitembelea Misri mwishoni mwa karne ya kumi au mwanzoni mwa karne ya kumi na moja BK.

Katika kipindi hiki Misri ilikuwa chini ya utawala wa Kifatimi, tangu 358 Hijria / 969 WK, wakati Jawhar Al-Siqili alipofika Misri kutoka Maghreb na akafika Alexandria na kuiteka, kisha akaendelea na safari yake kwenda Giza, na akaondoa upinzani wa Ikhshidi ulioandaliwa kwa kupigana naye, na akaingia mji wa Fustat na akashinda, na utawala wa Kifatimi uliendelea huko Misri hadi 567 AH / 1171 WK (الأحمر Al-Ahmar, 2012: 29).

#### 3.2.3.2 Vipengele vya Kisiasa Katika Misri Kupitia Riwaya ya *Mbali na Nyumbani*:

Ziara ya Shafi huko Cairo ilikuwa katika miaka ya 1960 - 1961 BK, na katika kipindi hiki mfumo wa kisiasa nchini Misri ulikuwa wajamhuri chini ya uongozi wa Marehemu Rais Gamal Abdel Nasser, ambaye alichukua madaraka mnamo 1954 AD hadi 1970 BK. Katika kipindi hiki, Nasser alichangia kuunga mkono harakati za ukombozi barani Afrika. Shafi aliashiria haya kwa kusema:

“Wakati huo Kairo ilikuwa chungu cha siasa ya Afrika... Siasa ilikuwa ikitokota sawasawa. Wananchi wa Afrika walikuwa wakidai uhuru. Vyama vya wapigania uhuru wa Afrika kutoka nchi mbalimbali vilijikusanya pamoja ndani ya nyumba nambari Kumi na Tano, Barabara ya Ahmed Hishmet, Mtaa wa Zamalek. Ndani ya nyumba hiyo kila chama cha kupigania uhuru kilikuwa na ofisi yake, na cha Zanzibar hivyo hivyo.” (Shafi 2013: 374).

Shafi alisisitizia hayo tena kwa kusema:

“Nyumba nambari Kumi na Tano iliyokuwepo Barabara ya Ahmed Hishmet ilikuwa ni nyumba iliyokuwa imejaa shughuli za kisiasa. Waliokuwemo, wote walikuwa wanaharakati wa kupigania uhuru wa nchi zao. Humo ilizungumzwa lugha moja tu, lugha ya ukombozi wa Afrika.” (Shafi 2013: 382).

Kupitia maneno ya Shafi, tunatambua kiwango cha msaada uliotolewa na Rais wa Misri Gamal Abdel Nasser wakati huo kwa harakati za ukombozi wa Afrika na mchango wake mkubwa katika kutokomeza ukoloni na kuimarisha uhuru wa nchi zao.

### **Hitimisho:**

Makala haya yalishughulikia taswira ya Misri katika riwaya za Kiswahili za kisasa. Riwaya mbili zimechaguliwa ili ziwe data za makala haya nazo ni; riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi, na riwaya ya *Siri Sirini* iliyoandikwa na Rocha Chimera. Katika utangulizi, mwandishi amezungumzia fasihi ya usafiri iliyoandikwa kwa Kiswahili kwa sababu aligundua kuwa aina nyingi za riwaya hizi zinaweza kufuata aina hii ya fasihi. Makala haya yana matokeo yafuatayo:

- 1- Motifu ya safari inaweza kuwa wazo kuu katika baadhi ya kazi za fasihi, kama ilivyokuwa katika riwaya ya *Mabali na Nyumbani*, na inaweza kuwa wazo lisilo kuu, kama ilivyokuwa katika riwaya ya *Siri Sirini*.
- 2- Ikiwa motifu ya safari ni wazo kuu katika kazi ya fasihi, msuko msago hutumiwa ambao matukio yake huwa ni ya moja kwa moja, kama ilivyotokea katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*.
- 3- Ikiwa motifu ya safari sio wazo kuu, basi msuko rudufu hutumiwa, kama ilivyotokea katika riwaya ya *Siri Sirini*.
- 4- Ikiwa mwandishi ndiye mhusika mkuu katika kazi ya fasihi, kama ilivyokuwa katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, basi kiambishi {Ni-} hutumiwa kuwakilisha nafsi ya kwanza (umoja) na kiambishi {Tu-} kuwakilisha nafsi ya kwanza (wingi).
- 5- Ikiwa mwandishi sio miongoni mwa wahusika wa kazi ya fasihi, kama ilivyokuwa katika riwaya ya *Siri Sirini*, basi kiambishi {A-} hutumiwa kuwakilisha nafsi ya tatu (umoja) na kiambishi {Wa-} kuwakilisha nafsi ya kwanza (wingi).

- 6- Chimera alielezea alama za Kimisri ambazo wajumbe wa Shanga walizona wakati wa ziara yao kwa Misri katika karne ya kumi BK, kama vile: Mji wa Cairo, Mto wa Nile, Ikulu ya Ufalme, Bustani ya Ikulu ya Ufalme, Mapiramidi ya Giza na Alexandria.
- 7- Shafi alielezea alama za Kimisri ambazo yeye mwenyewe alizona wakati wa safari yake kwenda Misri mnamo mwaka 1961, kama vile: Mashamba ya Misri ya Juu, Mji wa Cairo, Mto wa Nile, na Mji wa Port Said.
- 8- Chimera na Shafi walionesha vipengele vya maisha ya kijamii, kiuchumi na kisiasa nchini Misri kwa njia halisi inayolingana na kipindi ambacho matukio ya riwaya zao yalitukia.



**Marejeleo ya Kiarabu:**

- إبراهيم، رجب عبد الجواد، (2002) "المعجم العربي لأسماء الملابس في ضوء المعاجم والنصوص الموثقة من الجاهلية حتى العصر الحديث"، دار الآفاق العربية، القاهرة.
- Ibrahim, Rajab Abdel-Gawad (2002) "*Al-Mujam Al-Arabi Li-Asmaa Al-Malabis fi Dhuu Al-Maajim Al-Mauthuqah Min Al-Jahiliyah Hatta Al-Asr Al-Hadiith*", Dar Al-Afaaq Al-Arabiyah, Cairo.
- إبراهيم، محمد أحمد، (2007) "تطور الملابس في المجتمع المصري من الفتح الإسلامي إلى نهاية العصر الفاطمي 567- 20هـ / 1171-640م دراسة تاريخية، مكتبة مدبولي، القاهرة.
- Ibrahim, Muhammad Ahmad, (2007) "*Tatwur Al-Malabis fi Al-Mujtama Al-Misri Min Al-Fathil Islami Ila Nihaytul Asr Al-Fatimi (20-567 AH / 640-1171 BK) Dirasah Tarikhiya*", Maktabat Madbouly, Cairo.
- ابن حوقل، أبي قاسم بن حوقل النصي، (1992) "كتاب صورة الأرض"، دار مكتبة الحياة، بيروت لبنان.
- Ibn Hawqal, Abu Qasim Bin Hawqal Al-Nasi (1992) "*Kitab Swuratul Ardhi*", Dar Maktabat Al Hayat, Beirut, Lebanon.
- أحمد، نريمان عبد الكريم، (1993) "المرأة في مصر في العصر الفاطمي"، الهيئة المصرية العامة للكتاب، القاهرة.
- Ahmad, Nariman Abdel Karim, (1993) "*Al-Maratu Fi Misr Fi Al-Asr Al-Fatimi*", Al-Hayiah Al-Misriyah Al-Ammah LilKitab, Cairo.
- الأحمر، رمضان محمد رمضان، (2012) "الحياة الاجتماعية في مصر في عصر الدولة الفاطمية، 567- 358هـ / 1171-969م"، شركة القدس للنشر والتوزيع، القاهرة.
- Al-Ahmar, Ramadan Muhammad Ramadan, (2012) "*Al-Hayah Al-Ijtimaaiyah Fi Misr fi Asr Al-Dawlah Al-Fatimiyah, (358-567 AH / 969-1171 AD)*", Sharikat Al-Quds Lil-Nashr Wat-Tawzii, Cairo.
- بركة، ماجدة، (2009) "الطبقة العليا المصرية بين الثورتين 1952 – 1919 م"، ترجمة: محمود ماجد، المركز القومي للترجمة، القاهرة.
- Barakah, Magdah, (2009) "*Al-Tabaka Al-Uliya Al-Misriyah Baina Ath-Thawratayn (1919 - 1952 BK)*", tafsiri ya: Mahmoud Majed, Al-Markaz Al-Qawmi Lil-Tarjamah, Cairo.
- زكي، عبد الرحمن، (1966) "القاهرة تاريخها وأثارها 1825- 969 م من جوهر القائد إلى الجبرتي المؤرخ"، دار الطباعة الحديثة، القاهرة.
- Zaki, Abd al-Rahman, (1966) "*Al-Qahirah Tarikhaha wa Atharaha (969-1825 BK) Min Jawhar Al-Qaid Ila Al-Jabarti Al-Muarikh*", Dar Al-Twabiah Al-Hadithah, Cairo.
- سليم، أحمد أمين (1989) "في تاريخ الشرق الأدنى القديم مصر – سورية القديمة"، دار النهضة للطباعة والنشر، بيروت.
- Selim, Ahmed Amin, (1989) "*Fi Tarikh Al-Sharq Al-Qadiim, Misri - Siria Al-Qadiimah*", Dar Al-Nahdha LilTwibaah Wal Nashr, Beirut.
- شيحة، مصطفى عبد الله، (1988) "دراسات في العمارة والفنون القبطية"، مطبعة هيئة الآثار المصرية، القاهرة.
- Shiha, Mustafa Abdullah, (1988) "*Dirasaat Fi Al-Imarah wal Funuun Al-Qibtwayyah*", Matwbait Haiatul Athaar Al-Misriyah, Cairo.
- الطرابيلي، عباس، (1996) "شوارع لها تاريخ، سياحة في عقل الأمة"، الدار المصرية اللبنانية، القاهرة.
- Al-Tarabili, Abbas (1996) "*Shawarii laha Tarikh, Siyaha Fi Aql Al-Ummah*", Ad-Dar Al-Lebananiyah Al-Misriyah, Cairo.
- عبد الجواد، توفيق أحمد، (1984) "العمارة وحضارة مصر الفرعونية"، مكتبة الأنجلو المصرية، القاهرة.

Abd Al-Jawad, Tawfiq Ahmed, (1984) “*Al-Imarah wa Hadharit Misr Al-Faruniyah*”, Maktabat Al-Anglo Al-Misriyah, Cairo.

عشوب، عبد العليم، (2013) " تاريخ تربية الخيول العربية في مصر"، الدار العربية للموسوعات، بيروت.

Ashoub, Abdel-Alim, (2013) “*Tariikh Tarbiyat Al-Khuyul Al-Arabiyyah Fi Misri*”, Ad-D Al-Arabiyyah Lil-Mawsuaat, Beirut.

علماء الحملة الفرنسية، (1992) "وصف مصر"، الجزء الأول، ترجمة زهير الشايب، دار الشايب للنشر، القاهرة.

Wasomi wa Kampeni ya Ufaransa, (1992) “*Wasfu Misr*”, *Sehemu ya 1, tafsiri ya Zuhair Al-Shayeb*, Dar Al-Shayeb Lil-Nashr, Cairo.

القزويني، زكريا بن محمد بن محمود، (دت) "آثار البلاد وأخبار العباد"، دار صادر، بيروت، لبنان.

Al-Qazwini, Zakaria bin Muhammad bin Mahmoud, (Pasipo na tarehe) “*Athar Al-Bilaad Wa Akhbar Al-Ibaad*”, Dar Sader, Beirut, Lebanon.

قلا، إبراهيم علي السيد، (2007) " تاريخ مصر الاسلامية وجوانب من حضاراتها: منذ الفتح الإسلامي حتى نهاية العصر الفاطمي، 20-567 هـ 640-1171م"، مكتبة العلم والإيمان للنشر والتوزيع، القاهرة.

Qula, Ibrahim Ali Al-Sayed, (2007) “*Tariikh Misri Al-Islami Wa Jawanib Min Hadharataha: Mundhu Al-Fathul Islami Hatta Nihaytul Asr Al-Fatimi, 20-567 AH / 640-1171 BK*”, Maktabat Al-Ilm Wal-Imaan Lil-Nashr Wat-Tawzii, Cairo.

كيلاني، محمد سيد، (2010) " ترام القاهرة دراسة تاريخية، اجتماعية، أدبية"، الهيئة العامة لقصور الثقافة، القاهرة.

Kilani, Mohamed Said, (2010) “*Tram Al-Qahira Dirasah Tarikhiya, Ijtimaiyyah, Adabiyah*”, Al-Haiyyah Al-Ammah Liqusuur Ath-Thaqafah, Al-Qahirah.

ماجد، عبد المنعم، (1955) " نظم الفاطميين ورسومهم في مصر"، مكتبة الأنجلو المصرية، القاهرة.

Majid, Abd Al-Moneim, (1955) “*Nudhum Al-Fatimiin Wa Rusumahm Fi Misr*”, Maktabat Al-Anglo Al-Misriyah, Cairo.

مقداد، خليل، (2008) " الفسيفساء السورية والمعتقدات الدينية القديمة والميثولوجيا"، المديرية العامة للآثار والمتاحف، دمشق، الجمهورية العربية السورية.

Miqdad, Khalil, (2008) “*Al-Fusaifisaa As-Suriyah Wal-Mutaqadaat Ad-Diniyyah Wal-Mitholojia*”, Al-Mudiriyyatul Ammah Lil-Athaar wal Mataahif, Dameski, Al-Jamhuriyyh Al-Arabiyyah As-Suriyyah.

### **Marejeleo ya Kiswahili na ya Kiingereza:**

Chami, Felix A. (2002) “*East Africa and the Middle East relationship from the first millennium BC to about 1500 AD*”, Tanzania, University of Dar-es-Salaam, Journal des Africanistes 72 (2) 2002: 21-37.

Chimera, Rocha, M. (2013) “*Siri Sirini (Mshairi na Mfungu)*”, Kitabu cha kwanza, Sasa Sema Publications, Nairobi.

Habwe, John, (2011) “*Safari ya Lamu*”, Sasa Sema Publications, Nairobi.

Harrow, Kenneth W. (1991) “*Faces of Islam in African Literature, Studies in African Literature: New Series*”. Portsmouth, New Hampshire: Heinemann, London.

Kayamba, H.M., (1932) “*Tulivyoona na Tulivyofanya Ingereza*”, Sheldon Press, England.

Levtzion, Nehemia & Pouwels, Randall, (2000) “*The History of Islam in Africa*”, Ohio University press, The United States of America.

Madumulla, Joshua S. (2009) “*Riwaya ya Kiswahili; Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*”, Mtire Educational Publishers Ltd, Dar es Salaam, Toleo la Kwanza, Tanzania.

- Mbatia, Mwenda, (2001) *“Kamusi ya Fasihi”*, Standard Textbooks Graphics and Publishing, Nairobi.
- Mulokozi M.M., Sengo T.S.Y. (1995) *“History of Kiswahili poetry, A.D. 1000-2000: a report”*, Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam, Tanzania.
- Reusch, Richard, (1961) *“History of East Africa”*, F. Ungar Pub. Co., New York.
- Shafi, Adam, (2013) *“Mbali na Nyumbani”*, Longhorn Publishers, Nairobi.
- Velten, C., (1901) *“Safari za Wasuaheli”*, Göttingen, Vandenhoeck & Ruprecht, Berlin.
- Wamitila, K.W. (2008) *“Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi”*, Vide-Muwa Publishers, Nairobi.
- Yanjela, David Wafula, (2017) *“Narrated Histories in Selected Kenyan Novels, 1963-2013”*, Dissertation presented for the degree of Doctor of Philosophy in the Faculty of Arts and Social Sciences at Stellenbosch University Stellenbosch University, South Africa.